

(29)

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Tel. 025-2530404

FAX NO. 025-253023



S.L.P 73,
TUNDUMA.
SONGWE- TANZANIA.

KUMB. NA. TTC/01/94/40

22/ 03/2018

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma kwa Mujibu wa Kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu (Utumishi) chenye Kumb.Na.CFC 26/205/01 "F"/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017, anawatangazia wananchi wote nafasi za Kazi ya **Mtendaji wa Mtaa III** Watakaopangiwa kufanya kazi katika Mitaa ya Mji wa Tunduma.

1. Idadi ya Nafasi (Nafasi 07)

2. Majukumu ya Mtendaji wa Mtaa III

- i. Kuwa Katibu wa Kamati ya Mtaa
- ii. Kuwa Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- iii. Kuwa Mratibu wa Utekelezaji wa Sera na Sheria zinazoteklezwa na Halmashauri katika Mtaa
- iv. Kuwa Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- v. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria Ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa
- vi. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- vii. Msimamizi ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote katika Mtaa anatakaofanyia kazi
- viii. Kuandaa na kutunza rejestra ya wakazi wote wa Mtaa wake

3. Sifa za Mwombaji

- i. Awe raia wa Tanzania
- ii. Awe amehitimu na kufaulu Elimu ya Kidato cha IV na zaidi na vyeti vyake viwe halali visivyo na shaka yoyote.
- iii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za

Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

iv. Awe na Umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45.

4. Aina ya Ajira na Maslahi ya Nafasi hii;

Ajira hii ni ya Masharti ya KUDUMU (Permanent & Pensionable) na Mshahara wake utakuwa katika ngazi ya TGS B.1 sawa na Sh. 390,000/= kwa mwezi.

5. Mwajiriwa atakuwa anasimamiwa na Mtendaji wa Kata na atawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma.

6. Nyaraka za Kuambatisha kwenye Maombi

- i.Taarifa binafsi (C.V)
- ii.Nakala za Vyeti vya Elimu na Mafunzo
- iii.Cheti cha kuzaliwa
- iv.Mawasiliano (*hususani namba za simu-Mobile*)
- v.Picha 2 za rangi (*passport size*)

7. Muda wa Kutuma Maombi ni kuanzia tarehe **23 Machi hadi 08 Aprili, 2018 Saa 9.30 Alasiri. Baada ya hapo Maombi hayatapokelewa.**

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi wa Mji

Halmashauri ya Mji

S.L.P 73

TUNDUMA (Mawasiliano-)

Limetolewa na:-

Rita J. Kamenya

**KAIMU MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI**

